# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA ARDHI NA MAWASILIANO KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI KWA MWAKA 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuturuzuku uhai na afya njema na kuweza kufika hapa kwa lengo la kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru wewe binafsi kwa niaba ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa kuniruhusu kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumzi kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kumshukuru pia Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo kwa mashirikiano makubwa waliyotupatia wakati wa kuchambua na kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe na Makatibu wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa busara zao na mashirikiano yao ya dhati waliyoyaonesha na hatimae Kamati hii ikaweza kuipitia, kuichambua na kutoa mapendekezo yake kwa lengo la kuimarisha utendaji wa Wizara hii ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba sasa kuwataja Wajumbe na Makatibu wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kama ifuatavyo:

1. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mwenyekiti.
2. Mhe. Suleiman Sarhan said - Makamo Mwenyekiti.
3. Mhe. Khadija Omar Kibano - Mjumbe
4. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Mjumbe
5. Mhe. Hidaya Ali Makame - Mjumbe
6. Mhe. Said Omar Said - Mjumbe
7. Mhe. Ussi Yahaya Haji - Mjumbe
8. Ndg. Fatma Omar Ali - Katibu
9. Ndg. Mwaka Mwinyi Waziri - Katibu

**Mheshimiwa Spika,** baada ya shukurani hizo naomba sasa niende moja kwa moja kwenye uwasilishaji wa Hotuba ya Maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

## PROGRAMU KUU YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI

**Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu hii inasimamiwa na programu ndogo tatu ambazo ni Programu ndogo ya Usimamizi wa Usafirishaji, Programu ndogo ya Miundombinu ya Usafirishaji na Programu ndogo ya Huduma za Usafirishaji.

## PROGRAMU NDOGO YA MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inampongeza sana Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuendeleza Ujenzi wa Barabara za Unguja na Pemba ikiwemo Ujenzi wa Barabara ya Ole - Kengeja ambayo iko mbioni kukamilika hali inayowapunguzia sana wananchi

usumbufu wa mawasiliano baina ya mji na mji ambapo imeunganisha mawasiliano baina ya Chake kuelekea Kengeja na Kiwani .

**Mheshimiwa Spika,** kupitia programu ndogo hii Kamati imegundua kuna ucheleweshaji wa ukamilishaji wa Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Ole - Kengeja (Pemba) hali inayowasababishia usumbufu mkubwa wananchi wanaotumia barabara hii. Aidha, kitendo hiki kinamvunja moyo Mheshimiwa Rais wetu Mpendwa kwa kuchelewa kwa ukamilishaji wa Ujenzi wa Mradi huo kabla ya kumalizika kwa Uongozi wake kwani kufanya hivyo ni wazi kunarudisha nyuma azma na malengo yaliopangwa kutekelezwa kama Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi inayoelekeza.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuipitia bajeti hii Kamati imebaini kuwa kuna ucheleweshwaji wa ulipaji wa fidia kwa wananchi walioathirika na Mradi wa Ujenzi wa Barabara hii kwa kuathiriwa kwa makaazi pamoja na vipando vyao bila ya kulipwa chochote, hali inayopelekea malalamiko makubwa kwa wananchi na kutokuiamini Serikali yao.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na Kadhia hii, Kamati inaiomba Serikali kuharakisha zoezi zima la ulipaji wa fidia kwa wananchi ili kuyaondosha malalamiko yaliopo na kujenga imani kwa nchi yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Utanuzi wa Barabara ya Ole - Kengeja umepelekea kuwepo kwa matumizi yasio sahihi ya kisima na Msikiti katika eneo ambalo mradi unatekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Hivyo, Kamati yangu inaiomba Wizara ya Ujenzi kwa Kushirikiana na Mamlaka ya Maji (ZAWA) kulitafutia ufumbuzi suala la Maji ili kuwaondolea

changamoto wananchi wanazokumbana nazo hivi sasa katika Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Unguja Kamati yangu pia inampongeza Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuondoa kadhia na kilio cha muda mrefu wa watu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa kuwatandazia mtandao wa Barabara ya kisasa na ya aina yake. Barabara ya Bububu - Mkokotoni ambayo imejengwa kwa kiwango cha Kimataifa tunaamini watu wa Mkoa wa kaskazini hawatomsahau maisha yao Dk.Shein kwa kuona kilio chao cha muda mrefu na kuweza kukitatua ndani ya awamu yake ya Uongozi, pia Madaraja yaliyojengwa kwenye barabara hiyo ni ya kisasa na ya kiwango cha hali ya juu tunaamini wananchi wa Kaskazini mwaka huu watamimina kura zote kwa CCM ili iwe shukrani zao kwa Dk. Shein kwa kuwajali.

**Mheshimiwa Spika,** Pia katika Mkoa huo huo wa Kaskazini Unguja ameweza kuwajengea Barabara ya Pale - Kiongele ambayo itarahisisha mawasiliano baina ya watu wa Mkwajuni na Donge ambapo pia itaondoa msongamano katika Barabara ya Mkokotoni kwa kutumia Barabara hii, ila Kamati yangu inaiomba Serikali kuangalia uwezekano kuweza kumuongezea mkataba Mkandarasi anaejenga Barabara ya Bububu - Mhonda - mkokotoni kuimalizia kipande kilichobaki kinachotoka Mkokotoni kupitia Donge hadi Mahonda kwani kipande hicho hakitoi sura nzuri ya mtandao wetu wa Barabara ya Kaskazini kwa hiyo Kamati yangu inamuomba Mhe. Rais kumuongezea mkataba mjenzi ili akimalizie kipande hiyo ili kiu ya wananchi wa Kaskazini imalizike kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inampongeza Mhe Rais kwa kuiunganisha Barabara ya Matenwe Mbuyu Tende kwani barabara ile imeliongezea haiba na thamani eneo lile

ambalo ni muhimu kwa uwekezaji lakini pia kwa wananchi wa Matemwe naamini na wao watalipa fadhila kwako kwa kuwaona na kufanya jambo lenye faraja katika kuwaondolea umaskini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa kuwajali wananchi wetu kwa kutandandaza mtandao wa Barabara ambapo zikimalizika Barabara hizi zinazoendelea hapa Unguja ikiwemo Koani - Jumbi, Fuoni - Kombeni ambazo zikimaliza zitapunguza msongamano wa Magari katika eneo lka Mwanakwerekwe lakini pia litarahisisha kupunguza masafa ya kutoka Kusini, Kaskazini kujia Fumba.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu pia inampongeza Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuondoa kadhia ya muda mrefu kwa ujenzi wa Daraja la Kibonde Mzungu Daraja ambalo kwa miaka mingi limekua likileta usumbufu mkubwa kwa kujaa Maji na Magari kushindwa kupita kutokana na kiwango cha Maji yanavyojaa, pamoja na hayo kumejitokeza kujaa Maji katika mitaa ya jirani na Daraja hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inaiomba Serikali kupitia tume ya Mipango kuandaa mradi maalum wa kufanya uchambuzi yakinifu ili kuangalia njia ya kuyaondoa Maji yale na kuyapeleka Baharini au kushirikiana na Mamlaka ya Maji (ZAWA) kuangalia uwezekano wa kujenga Bwawa ambalo litatumika wakati wa Kiangazi kumwagilia mashamba ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Pia, Kamati yangu inaitaka Wizara kushirikiana na Tume ya Mipango kuandaa mradi ambao utaweza kujenga Daraja au njia mbadala ya kuyaaondoa Maji yanayojaa kila zinaponyesha Mvua kubwa za Masika katika eneo la Dunga ambalo Maji

hujaa sana na kuifanya Barabara ya Dunga kufungwa kutokana na kufunika kwa maji ya mvua jambo ambalo linaleta usumbufu kwa wakaazi wa eneo hilo na pia wanaopita kwa Magari.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu pia inaipongeza Wizara kwa kulitekeleza agizo alilolitoa Mhe. Rais wakati alipokuja kufungua Daraja la Kibonde Mzungu, agizo alilosema kua kipande cha Barabara ya kutoka Kituo cha Polisi - Fuoni hadi kwenye Daraja hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Tunaishukuru Wizara kupia Waziri na kumuagiza Katibu Mkuu na kipande hicho hivi sasa kiko katika hatua za mwisho kukamilika. Wizara imeonyesha mfano wa kuigwa na taasisi nyengine Mhe. Rais anapotoa agizo basi litekelezwe mara moja. Kamati yangu inampongeza Mkandarasi Mzalendo wa Kampuni ya MECCO ambayo ilipewa kazi hiyo kuikamilisha amejitahidi kutekeleza agizo la Rais ingawa hadi hii leo bado hajalipwa hata senti moja lakini ameendelea na ujenzi bila ya kusita ingawa kulikuwa na mkwamo wa kuchelewa kuondolewa kwa baadhi ya Miundombini ikiwemo Umeme na Maji ambapo Kamati yangu ilisaidia kufanya mawasiliano na Meneja wa Shirika la Umeme na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maji (ZAWA) na kuharakisha kuondoa miundombinu yao.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na pongezi hizo kwa kuwa hii ndio Bajeti ya mwisho ya Wizara hii kwa Awamu hii ya Dkt. Ali Mohamed Shein tunaomba Wizara kuhakikisha Malipo ya Mkandarasi huyu Mzalendo yanalipwe kwa haraka ingawa hayakuwemo kwenye Bajeti ya Wizara lakini kwakuwa ni agizo la Mhe. Rais Waziri utakuja kutuambia utazilipa fedha hizo lini na kupitia vifungu gani, lakini pia kuna madeni ya ZECO na

ZAWA nayo pia katika Barabara hiyo Kamati yangu inaomba yalipwe kabla ya kumaliza mwaka huu wa Fedha.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu pia inashauri Idara ya Mipango kuharakisha uandaaji wa "Road Master Plan" kwani kasi ya ujenzi katika Nchi yetu inaongezeka siku hadi siku kwa hiyo ujenzi wowote lazima uangalie "Road Master Plan" inasemaje.

**Mheshimiwa Spika,**

Mradi wa Jengo jipya wa Terminal III kama tujuavyo mradi huu ni wa muda mrefu ulikwama kutokana na sababu mbali mbali lakini tunashukuru kua hivi sasa mradi huu unaendelea vizuri. Kamati yangu inamtaka Mkandarasi kuharakisha ujenzi huo ili tuweze kuuzindua mapema iwezekananvyo. Kamati yangu inaamini Uwanja huu wa Terminal III ukimaliza utaweza kuongeza ajira nyingi lakini pia utaweza kuhamasisha Makampuni ya Ndege makubwa kuja kuleta ndege zao kutumia kiwanja chetu.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hayo Kamati yangu inaitaka Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuanza kuwapeleka kwenye mafunzo mapema wafanyakazi ambao watakao kuja kufanya kazi hapo kwani Uwanja huu utakua wa kisasa na vifaa vya kisasa kwa hiyo lazima kuwe na mpango madhubuti ya maandalizi kwa wafanyakazi katika Uwanja huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inampongeza sana Msimamizi Mkaazi wa Ujenzi huo Ndugu YASSIR DECOSTER kwa kazi kubwa nzuri na ya Kizalendo aliyoionyesha wakati wote wa mradi huo ili kuhakikisha maslahi ya nchi yanasimamiwa ipasavyo ili kupata

Kiwanja kilicho bora, Ndugu DECOSTER aliweza kuvumilia wakati wote wa kipindi cha mripuko wa Maradhi ya COVID 19 ambapo waswahili wote waliondolewa na Mkandarasi wa Kichina kwa kuhofia kuambukizwa maradhi ya CORONA lakini Ndugu DECOSTER yeye aliendelea kubaki na wachina hao kusimamia kazi ili iende kama ilivyokusudiwa,

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inamuomba Mhe. Waziri baada ya kumaliza ujenzi huo Ndugu DECOSTER apewe tunzo maalum ya utumishi uliotukuka kwa kuonyesha Uzalendo na Uvumilivu katika muda wote wa Ujenzi wa Uwanja huo.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Mpiga Duri Kamati yangu inaiomba Wizara kuharakisha taratibu za kumpata Mshauri Muelekezi ili ili kupata makisio halisi ya kina ili mradi huo uweze kutekelezwa, Kamati yangu inachosikika ni kwamba miradi ya wenzetu Tanzania Bara inabuniwa katika kipindi kifupi na inatekelezwa kwa kasi kubwa lakini ya kwetu sisi inachukua muda mrefu kutekelezwa jambo ambalo wananchi wetu w

**PROGRAMU NDOGO YA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI**

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Meli Kamati yangu inasikitika na mitihani inayolikumnba Shirika kila kukicha kutokana na maharibiko ya Meli zake zote ikiwemo MV. Maendeleo, Mapinduzi na Uombozi I na II pamoja na hayo Kamati yangu inaiomba Serikali kuhakikisha Mapato ya Shirika yanatumika katika kuzihudumia Meli wakati wowote kunapohitajika matumizi, lakini pia Kamati yangu inaiomba Serikali kupitia Tume ya Utumishi kushughulikia maslahi ya wafanyakazi wa Shirika ili kuwapa moyo wa kujituma ili waweze kutoa huduma bora. Kamati yangu inaitaka Tume ya utumishi kuzingatia kada

ya Manahodha na Mabaharia kwani kada hizi ni tofauti na kada nyingine kwa hiyo ni vyema kuzingatia maslahi yao.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) Kamati yangu bado inaitaka Serikali kuangalia namna ya kuiwezesha Mamlaka hiyo ili iweze kukusanya baadhi ya tozo na ada ili kuweza kujiendesha lakini pia kuifanya ZMA kua wakala pekee wa usafirishaji na utoaji mizigo ya Serikali kama ilivyo Tanzania Bara jambo ambalo litaweza kuisaidia Mamlaka kimapato lakini pia kudhibiti mianya ya matumizi mabaya ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu pia inapongeza ZMA kwa uvumilivu mkubwa ambao wameuonyesha tangu kuzuiwa kusajili Meli za nje kwani eneo hilo ndilo lilikua ni uti wa mgongo wa mapato yote ya Mamlaka.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na hayo bado Kamati yangu inamuomba Mhe Waziri asichoke aende kuonana na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuweza kulisawazisha tatizo lililojitokeza katika usajili wa Meli za Nje kwani sisi Zanzibar kwa mazingira yetu ya Visiwa basi moja ya vianzio vyetu vya mapato ni matumizi mazuri ya Bahari yetu na kuzitumia fursa zitokanazo na kujaaliwa na kua na Bahari ikiwemo na fursa ya usajili wa Meli za Kigeni ili kuongeza mapato ya nchi.

**MheShimiwa Spika,** Kamati yangu pia inalipongeza Shirika la Bandari kwa kazi kubwa wanazozifanya kwa kuhudumia Meli za Abiria na Mizigo, pongezi hizo zinakuja kutokana na kupungua changamoto iliyokuwepo ya kulundikana kwa Makontena hapo

Bandarini Unguja lakini bado Kamati yangu inalishauri Shirika kujenga eneo la dharura kwa muda katika eneo la Maruhubi ili kuwekea Makontena kwa ni bado eneo letu la Bandari ni dogo na haliongezeki lakini pia pale Bwawani ni pahala pa muda tu sasa lazima tuhakikishe Shirika linaandaa mradi maalumu wa kujenga Bandari kavu huko Maruhubi ili kuhakikisha Meli zozote kubwa ziweze kuteremsha Makontena na kupakia bila ya usumbufu kwani kuchelewa kwa Meli kupakia au kuteremsha mizigo inapelekea Meli nyengine kukimbia na kuteremsha mizigo yao hasa Makontena katika Bandari jirani jambo ambalo linaikosesha Serikali mapato.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo, Kamati inaiomba tena Serikali kulipatia Shirika la Bandari eneo mbadala la uwekaji wa makontena nje ya Bandari ili kupunguza mlundikano wa makontenao kwa lengo la kurahisisha shughuli za kiutendaji ndani ya Shirika hilo.

## PROGRAMU KUU YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa kupitia Programu ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu ya TEHAMA na Programu ndogo ya Usimamizi wa Huduma za TEHAMA.

## PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI WA MIUNDOMBINU YA TEHAMA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa kuanzishwa kwa wakala wa Mkonga wa Mawasiliano ambapo kasi ya Mkurugenzi imetutia moyo sana ambapo katika kipindi kifupi tumeshaanza kuona matunda yake hasa kutokana na mapato makubwa ambayo Serikali imeanza kuyapata kutoka Kampuni ya Zantel ambapo kwa

miaka mingi ya nyuma mapato hayo yalikosekana, Kamati yangu inaitaka Wakala huyo aongezewe nguvu ya kuziunganisha taasisi zote za Serikali na binafsi kama alivyoanza ili kupatikana huduma bora za mawasiliano lakini pia kuunganisha mifumo yote ya kodi za Serikali, Kamati yangu inaitaka Wakala apewe nguvu za kuunganisha mkongo wa mawasiliano katika Mahoteli yote ya kitalii kwani huko kuna mapato mengi yanayovuja kutokana na Serikali kutokua na mfumo madhubuti wa kufuatilia na kuona mapato ya kwenye mahoteli hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inaamini kuwa Wakala akiweza kuunganisha mifumo ya kodi katika Viwanja vya Ndege, Bandari, Kwenye Mahoteli pamoja na Mabenki basi tunaamini mapato ya Serikali yataongezeka zaidi ya mara mbili , isitoshe pia katika huduma hasa katika Hospitali zetu itakuwa rahisi kujua mahitaji ya Madawa katika kila Hospitali na Vituo vya Afya na kuweza kutoa huduma zilizobora.

**Mheshimiwa Spika**, Wenzetu Mombasa Kenya wameunganisha mifumo yao yote ya Bandari na Mamlaka ya Kodi TRA ambapo hapo zamani wafanya biashara walikua huchukua kiasi siku kumi kuweza kukamilisha kulipia Makontena yao ili kuyatoa Bandarini na wafanya Biashara walikua wanakwenda kugongwa mihuri kwenye taasisi zaidi ya nane (8) ili kukamilisha malipo na kutoa mizigo yao Bandarini lakini hivi sasa tangu kuunganishwa na Mkongo wao wa Taifa na kutengenezewa mifumo ya kodi basi imekuwa mfanyabiashara anaweza kukamilisha malipo yote katika taasisi zote wakati yuko ofisini kwake ndani ya siku moja na kuweza kutoa Makontena yake hapo Bandarini bila ya kwenda popote. hii imesaidia sana kuondoa urasimu lakini kubwa zaidi kuongeza uwazi na mapato halisi ya kodi kwa Serikali kwa hiyo na sisi ni vyema kujifunza kwa

wenzetu ambao hata Shirika lenyewe la Bandari wameweza kuongeza mapato mara dufu na hivi sasa wameweza kutanua na kujenga Bandari zao zote kwa wakati mmoja ile ya Mombasa, Lamu na kwenye Lake Victoria hii yote inatokana na mapato kuongezeka lakini pia wanaweza kupata mikopo ya moja kwa moja kupitia Mashirika ya Kimataifa na kuweza kujenga miundombinu yao na kuongeza mapato ya Shirika kwa hiyo na sisi lazima tuige mazuri ambayo wenzetu wanayoyafanya.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu pamoja na mazuri hayo haijaridhika na eneo ambalo linatumika kama "DATA CENTRE" Mazizini kwani eneo lenyewe ni dogo lakini pia kiusalama halipo katika position nzuri kwa "DATA CENTRE" katika ulimwengu wa sasa ndio uti wa mgongo wa uchumi wa Nchi, kwa hiyo Kamati yangu inaiomba Serikali kuharakisha ujenzi wa "DATA CENTRE" mpya huko Tunguu ambapo kuna eneo la kutosha kwa ajili yaujenzi huo ambapo unahitaji miundombinu mikubwa nay a Kisasa lakini pia ulinzi na usalama wa kutosha.

**Mheshimiwa Spika**, Mwisho kabisa Kamati yangu inaiomba Serikali kadri upatikanaji wa fedha unavyopatikana kuziingizia taasisi zetu fedha kwa wakati, kwa lengo la kuharakisha kasi ya mendeleo ya nchi na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kamati ya Ardhi na Mawasiliano imeyaridhia mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hivyo basi, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili wayapitie, wayajadili na hatimae wayapitishe Makadirio hayo ili Wizara hii izidi kutekeleza vyema majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nimalizie hotuba yangu hii kwa kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, kwa utulivu na umakini wao wa kunisikiliza wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

Ahsante,

……………………………

Hamza Hassan Juma,

Mwenyekiti,

Kamati ya Ardhi na Mawasiliano,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**